# RUANGWA DC

RUANGWA KWA MAENDELEO INAWEZEKANA TIMIZA WAJIBU WAKO

Kitengo cha Habari na Mawasilino Serikalini

JARIDA Toleo namba 01 Juni 2024 Tetembelea www.ruangwadc.go.tz ruangwadc

HALIUZWI


# Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Azindua Kituo cha Malipo Ruangwa



UK..01

## Watendaji, Maafi sa Ugani Waagizwa Kutimiza Majuku mu Yao Kikamilifu



### DC Ruangwa Azindua Huduma ya Umeme Kijiji cha Mmawa

>>UK 10



### Ruangwa DC Waadhimisha Siku ya Mazingira Duniani

>>UK 01



### Mkurugenzi Mtendaji Ruangwa Akagua Miradi

>>UK 08



HALIUZWI

Ruangwa DC



# Wilaya ya Ruangwa Yaadhimisha Siku ya Mazingira Duniani



Kuelekea kilele cha Maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani ambayo huazimishwa kila ifikapo June 5, kila mwaka Viongozi wa Wilaya ya Ruangwa kwa kushirikiana na wananchi wameanza maadhimisho hayo kwa kufanya mazoezi (jogging)na kufanya usafi eneo la wazi nyuma ya kwa Wanyumbani. Mazoezi na usafi umefanyika leo June 1, 2024 ambapo mazoezi( jogging) yamefanyika kwa zaidi ya kilomita 5 na usafi umefanyika eneo la mraba zaidi ya hekari 1 Kwa mwaka 2024 kilele cha Maadhimisho ya siku ya mazingira duniani kimataifa yatafanyika katika jiji la Riyadh nchini Saudi Arabia, yakiongozwa na kaulimbiu " Urejeshwaji wa Ardhi iliyoharibiwa na ustahimilivu wa hali ya jangwa na ukame" Kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha jamii kuwa na matumizi endelevu ya Ardhi pamoja na kukabiliana na uharibifu wa ardhi zinazopelekea kuenea kwa jangwa na ukame.

Na kitaifa maadhimisho haya yatafanyika katika kituo cha mkutano Jakaya Kikwete Jijini Dodoma ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi na kwa Mkoa wa Lindi kilele cha Maadhimisho kitafanyika katika Manispaa ya Lindi na mgeni rasmi atakayeshiriki shughuli za usafi anatarajiwa kuwa Mhe. Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Lengo la Maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani ni kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zake kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma ametoa wito kwa wananchi kufanya mazoezi pasi shuruti ili kuimarisha Afya na kufanya usafi katika mazingira yanayowazunguka kwani mazingira yakiwa safi na Afya ikiwa imara watakuwa wamejiepusha dhidi ya magonjwa mbalimbali.

**MAKALA MAALUM**

## Ruangwa DC yaadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika

Katika kukumbuka siku hii, Umoja wa nchi za Afrika mnamo mwaka 1991 ziliweka Azimio la kuifanya siku ya tarehe 16 Juni ya kila mwaka kuwa ni siku maalum ya kuwaenzi watoto mashujaa waliokufa kwa ajili ya kudai haki yao ya kuendelezwa kielimu bila ubaguzi na hivyo kuitwa siku ya Mtoto wa Afrika. Kuanzia hapo maadhimisho haya yamekuwa yakifanyika kila mwaka katika nchi na wanachama kwa kufanya tathimini kuhusu utoaji wa haki ya mtoto na huduma zinazohusu malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto. Chimbuko la siku ya Mtoto wa Afrika ni tukio la mauwaji ya watoto takribani 2,000 yaliyofanywa na Askari wa Utawala wa Makaburu katika Kitongoji cha Soweto nchini Afrika Kusini tarehe 16 Juni, 1976.

Mauaji hayo yalitokea wakati Askari hao wanazuia maandamano ya watoto waliokuwa wanapinga mfumo wa elimu ya kibaguzi iliyokuwa inatolewa na Utawala wa Makaburu. Kila mwaka, siku ya mtoto wa Afrika huadhimishwa ba kauli mbiu maalum inayolenga




eneo fulani la haki za watoto Kauli mbiu inayoongoza maadhimisho haya kwa mwaka huu 2024 ni " Elimu jumuishi kwa watoto izingatie maarifa, maadili na stadi za kazi"

## Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Azindua Kituo cha Malipo Ruangwa



Kufuatia mwendelezo wa Jukwaa la pili la maendeleo ya ushirika Mkoa wa Lindi 2024, Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Bi. Zuwena Omary kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa amezindua na kuweka jiwe la Msingi katika kituo cha malipo ya Wakulima leo June 4, 2024 kilichopo Lipande wilayani Ruangwa.

Kituo hicho ni msaada kwa Wakulima kwani kitawasaidia kupata stahiki zao za mazao karibu yao na ni kwenye ofisi yao maalum ukilinganisha na hapo awali ambapo walikuwa wanapata stahiki zao kutoka ghala kuu.

Kituo hicho kimegharimu zaidi ya Milioni 100 za kitanzania mpaka kukamilika kwake. Aidha Mhe. Zuwena Omary amemtaka Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma kuhakikisha kampeni ya upandaji miti inaendelea katika maeneo mbalimbali wilayani humo ili kupambana dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi halikadhalika kupendezesha na kuipamba Wilaya



# Mwenyekiti wa Halmashauri Awataka Watendaji na Maafisa Ugani Ruangwa Kutimiza Majukumu Yao Kikamilifu

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe ametoa wito kwa Watendaji Kata, Watendaji wa Vijiji na Maafisa ugani kupambana na kuwajibika ipasavyo na kila mmoja kutimiza majukumu yake bila shuruti ili iwe chachu ya maendeleo katika Vijiji, Kata na Halmashauri kwa ujumla.

" Mabadiliko ni hatua, na hatua hiyo inahitaji utayari na uthubutu, endapo kila mmoja atatimiza wajibu wake kikamilifu tutapata hayo mabadiliko ya maendeleo katika vijiji vyetu, Kata zetu, na Halmashauri yetu"

Hayo ameyasema leo Juni 18, 2024 katika Kikao kazi kilichohusisha Watendaji Kata, Watendaji wa Vijiji, Maafisa ugani kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

Aidha Mhe. Chikongwe amewataka Maafisa ugani Kata kujua idadi kamili ya wakazi katika Kata husika ili kuweza kufanya hesabu ya kiasi gani cha chakula kinahitajika na hekari ngapi zinapaswa kulimwa ili kupata mazao ya chakula yanayokidhi mahitaji ya wakazi. "Maafisa ugani hii ni kazi yenu, msisite kuwatembelea wakulima ili kuweza kuwafahamu kwa mmoja mmoja na kuwapa msaada wa kilimo bora cha kisasa kwa karibu kabisa kwa sababu hata hizo Korosho na Ufuta tunaoutegemea unalimwa na wananchi wa kawaida" Amesema Chikongwe.

> "Mabadiliko ni hatua, na hatua hiyo inahitaji utayari na uthubutu, endapo kila mmoja atatimiza wajibu wake kikamilifu.
> — Chikongwe



*Watendaji wa Vijiji, Kata na Maafisa Ugani wakiwa kwenye kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa leo Juni 18, 2024. Mgeni rasmi wa kikao hicho alikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa mhe: Andrew Chikingwe ambapo amewataka maafisa hao kutimiza majukumu yao ipasavyo. picha na mpiga picha wetu*



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe (aliye simama) akitoa wito kwa Watendaji Kata, Watendaji wa Vijiji na Maafisa ugani kupambana na kuwajibika ipasavyo ili kuleta maendeleo ndani ya Halmashauri , leo Juni 18, 2024 katika Kikao kazi kilichohusisha Watendaji Kata, Watendaji wa Vijiji, Maafisa ugani kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. picha na mpiga picha wetu*

## Chikongwe Ahitimisha Kambi ya UMISSETA 2024 Ruangwa



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe amehitimisha kambi ya UMISSETA 2024 leo June 4, 2024.

Kambi hiyo iliwekwa katika Shule ya Sekondari Ruangwa ambayo ilianza Mei 25, 2024 ikiwa na wanafunzi washiriki 216 kutoka shule mbalimbali na mpaka kufikia hatua ya kuhitimisha kambi hiyo wamebaki wanafunzi 120 pekee ambao wanaendelea kuiwakilisha Wilaya katika ngazi ya Mkoa. Aidha, Mhe. Chikongwe ametoa zawadi ya vitafunwa kwa wanafunzi hao kutoka ABJ Kizota Bakery, “Fahari ya Nandagala” ambavyo vitawasaidia kama vifungua kinywa kabla ya kuanza safari yao mapema kesho.

Kwa upande wake, Afisa Michezo Wilaya Ndugu Shaban Mchinama ametoa wito kwa wanafunzi wanaoshiriki mashindano hayo kutokukata tamaa ili kujihakikishia ushindi kwani Wilaya inawategemea na ina imani watarudi na makombe ya ushindi na wataendelea na mashindano katika ngazi ya Taifa ambayo, kwa mwaka huu yatafanyika mkoani Tabora.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa kambi ya UMISSETA Wilaya Mwalimu Grayson Francis Lukoya amesema wamefanya maandalizi ya kutosha katika michezo yote wanayokwenda kushiriki na kuahidi kuchukua ubingwa kwa kishindo.

## Kituo cha Afya Nandagala Chaazimisha Mwaka Mmoja wa Huduma za Upasuaji

“Tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwaongoza na kuwasimamia watoa huduma ya upasuaji katika kituo chetu hiki na mpaka kufikia leo hii wagonjwa zaidi ya 70 wamepatiwa huduma hiyo na kutoka wakiwa salama salmini, lakini pia pongezi kubwa kwa yule mteja wetu wa kwanza kabisa ambaye alikuwa na imani kubwa na watoa huduma wa kituo chetu cha Afya na kuwa balozi mzuri kwa wananchi wengine kuwaaminisha ya kwamba Wataalamu wetu wa Afya katika kituo hiki wanatoa huduma ya upasuaji kwa weredi mkubwa”

Hayo yamebainishwa leo Juni 17, 2024 na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe ambaye pia alikuwa mgeni rasmi katika Kikao cha maadhimisho ya kutimiza mwaka mmoja tangu kuanza kutolewa huduma ya upasuaji katika Kituo cha Afya Nandagala, kilichofanyika katika kituo hicho.

Kituo hicho kimefunguliwa December 27, 2016 na kuanza kutoa huduma kama Zahanati na ilipofika mwaka 2022, kikaboreshwa zaidi na kuanza kutoa huduma kwa jamii kama Kituo cha Afya.

Mpaka sasa Kituo kina jumla ya Watumishi 14 na zaidi ya wananchi 20,000 wanapata huduma kupitia Kituo hicho, huduma zinazotolewa ni pamoja na huduma ya kujifungua (kwa njia ya kawaida na upasuaji) ambapo zaidi ya wakinamama 700 wamejifungulia katika kituo hicho, huduma ya kuona wagonjwa wa nje(OPD), huduma ya nasaha na upimaji wa VVU, huduma ya IPD(Wodi ya wakibaba, wakimama na watoto) na huduma nyingine nyingi.

Huduma ya upasuaji kwa mara ya kwanza ilifanywa na Dkt. Paul Christian Mbinga akishirikiana na Wataalam wengine kwa Bi Fikiri Bakari mkazi wa kijiji cha Ng’au mnamo Juni 12, 2023.

Aidha, Mhe. Chikongwe amemuomba Mganga Mkuu wa Wilaya Dkt. Feisal Said kuhakikisha Kituo cha Afya Nandagala kinakuwa na daktari bingwa wa kinywa na meno na hii ni kufuatia hatua ya kituo hicho kupokea kiti maalum kwa ajili ya huduma hiyo.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Wilaya Dkt. Feisal Said ametoa wito kwa Watumishi wa Kituo cha Afya Nandagala kufanya kazi kwa bidii, kupambana na kushirikiana vyema na Wataalam kutoka ngazi ya Wilaya ili kuleta mafanikio makubwa. “Mkitaka mfanikiwe fanyeni makubwa kazini na siri ya kufanikiwa ni kupambana tu” amesema Dkt. Feisal.



*Mwenyeki wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe akizungumza kwenye maadhimisho ya mwaka mmoja wa huduma ya upasuaji inayotolewa na kituo cha Afya Nandagala kilichopo kata ya Nandagala. picha na mpiga picha wetu.*

SIKILIZA RUANGWA FM
88.4

ruangwadc
www.ruangwadc.go.tz
ruangwadc

## Mkoa wa Lindi Wapata Timu ya UMISSETA 2024

Mashindano ya UMISSETA 2024 ngazi ya Mkoa yametamatika kwa kuchaguliwa timu ya Mkoa wa Lindi yenye wanafunzi washiriki 110 na walimu 12 kutoka Halmashauri zote 6 ambao watakaa kambini kwa takribani siku nne kuanzia leo tarehe 9, Juni 2024 kabla ya kuendelea na mashindano hayo kwa ngazi ya Taifa.

Mashindano ya 50 ya UMISSETA ngazi ya Taifa kwa mwaka huu yatafanyika Mkoa wa Tabora kuanzia Juni 16 mpaka Juni 26.



*Wanafunzi wa Wilaya mbalimbali za Mkoa Lindi walioshiriki mashindano ya UMISSETA 2024 katika ngazi ya Mkoa wakiwa kwenye picha pamoja. hatua inayofuata nIi ngazi ya Taifa.*

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa UMISSETA Mkoa wa Lindi Ndugu Omath Sanga ametoa wito kwa Walimu waliochaguliwa kuifundisha timu ya Mkoa kuandaa timu yenye ushindani, nidhamu na kujituma.

Aidha, Ndugu Sanga amewataka Wanafunzi waliobahatika kuchaguliwa kuuwakilisha Mkoa katika mashindano ya UMISSETA 2024 kitaifa kujua kuwa wanadhamana ya kuuwakilisha vyema Mkoa wa Lindi katika michezo yote., hivyo basi wacheze kwa kujituma na kwa bidii zaidi ili kuufanya Mkoa wa Lindi uwe kinara kimichezo katika ngazi ya Taifa kiujumla.

# Mwenyekiti wa Halmashauri Akabidhi Mbuzi 10 kwa Wanakikundi cha Ukombozi Nandagala

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe amekabidhi mbuzi 10 wa kufuga leo Juni 20, 2024 kwa Kikundi cha Ukombozi kilichopo kijiji cha Nandagala wilayani Ruangwa

Mbuzi hao wamepatikana baada ya Baraza la NACOFA kutembelea kikundi cha Ukombozi Mwezi 11, 2023 na kuahidi kuchangia shilingi Milioni 2 ili kukiimairisha kikundi hicho kupitia shughuli mbalimbali.

Kikundi hicho kimeanzishwa mwaka 2022 kikiwa na jumla ya wanakikundi 16 kikiwa na lengo la kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali kama vile kilimo na ufugaji pia kuimarisha afya kwa kuzingatia lishe bora.

Aidha, Mhe. Chikongwe ametoa wito kwa wanakikundi kutilia maanani mradi huo ili kupata matokeo chanya ya kimaendeleo katika kijiji na Kata kwa ujumla.

“Wenzetu wanatusaidia na wanataka matokeo chanya, hivyo basi wekeni mkazo kuhakikisha mbuzi hawa wanaongeza thamani ya kijiji chetu na msiwe na haraka ya kupata matokeo, hii itasababisha kuvuruga malengo”

Katika hatua nyingine, Mhe. Chikongwe amesisitiza mbuzi




*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe amekabidhi mbuzi 10 wa kufuga leo Juni 20, 2024 kwa Kikundi cha Ukombozi kilichopo kijiji cha Nandagala wilayani Ruangwa. Mbuzi hao wamepatikana baada ya Baraza la NACOFA kutembelea kikundi cha Ukombozi Mwezi 11, 2023 na kuahidi kuchangia shilingi Milioni 2 ili kukiimairisha kikundi hicho kupitia shughuli mbalimbali.*

hao wakitunzwa vizuri watasaidia kupata samadi itakayosaidia katika shughuli za kilimo, pia kupata maziwa ambayo yatasaidia kuimarisha afya halikadhalika kusaidia wanakikundi kupata fedha mara baada ya mbuzi kuuzwa pindi watakapoongezeka.


Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kikundi cha Ukombozi Ndugu Siwazuli Ally Nkundi amelishukuru Baraza la NACOFA na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na kuahidi kuendeleza mradi huo ili iwe chachu ya maendeleo kwao na Wilaya kwa ujumla.

“

Mkitaka mfanikiwe fanyeni makubwa kazini na siri ya kufanikiwa ni kupambana tu

—Dkt. Feisal.

# Kumbuka Kujiandikisha Kuwa Mpiga Kura, Ndio Msingi wa Utawala Bora









# Habari Picha



*Pichani ni Kikundi cha Wanafunzi washiriki mashindano ya UMISSETA 2024 kutoka Wilaya ya Ruangwa wameibuka washindi katika mchezo wa Sanaa za ndani kwa ngazi ya Mkoa. Sanaa za ndani inajumuisha ngoma za asili na muziki wa kizazi kipya. Picha na mpiga picha wetu.*



*Kikosi cha timu ya wasichana kutoka Wilaya ya Ruangwa kilicho ibuka kidedea katika fainali za mpira wa Pete (Netball) kwa ushindi mnono wa magoli 36 kwa 31 dhidi ya timu ya Wilaya ya Kilwa. Mchezo huo umechezwa leo Juni 8, 2024 katika viwanja vya Ilulu mkoani Lindi. picha na mpiga picha wetu,*



*Kwenye picha ni Mwanafunzi aliyeshinda nashindano ya riadha Kuruthumu Alawi kutokea Shule ya Sekondari Mnacho wilayani Ruangwa. Mashindano ya UMISSETA 2024 katika ngazi ya Mkoa yamefanyika leo Juni 8, 2024 katika viwanja vya Ilulu, ambapo Ruangwa imekuwa mshindi wa riadha za wasichana za mita 200. Picha na mpiga picha wetu.*



*Timu ya mpira wa miguu ya wasichana kutoka Wilaya ya Ruangwa inayoshiriki mashindano ya Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) 2024 leo tarehe 6, Juni imeshinda mchezo wake wa kwanza goli 1-0 dhidi ya timu ya mpira wa miguu ya wasichana Mtama, Goli la ushindi limewekwa wavuni katika kipindi cha pili cha mchezo. Picha na mpiga picha wetu.*



*Wanafunzi waliochaguliwa kuiwakilisha Wilaya ya Ruangwa kimkoa katika mashindano ya UMISSETA 2024 katika mchezo wa mpira wa miguu wavulana wamewafunga goli 3-0 wanafunzi kutoka Halmashauri ya Mtama. Mchezo huo umepigwa leo June 6, 2024 katika viwanja vya Ilulu mkoani. Picha na mpiga picha wetu.*



*Timu ya UMISSETA 2024 kutoka Wilaya ya Ruangwa inayoiwakilisha Wilaya katika ngazi ya Mkoa kwa upande wa mpira wa pete imetinga fainali kwa kishindo baada ya kuwashushia kipigo kizito cha magoli 21 kwa 11 timu kutoka Wilaya ya Liwale. Mchezo huo umechezwa leo Juni 7, 2024 katika viwanja vya Ilulu mkoani Lindi. Picha na mpiga picha wetu.*



*Wanafunzi wanaoshiriki mashindano ya UMISSETA kutoka Timu ya Netball Wilaya ya Ruangwa wameendelea kuonesha ubabe wao dhidi ya wanafunzi kutoka Halmashauri ya Mtama kwa kuwafunga goli 27 kwa 21 leo Juni 6, 2024. picha na mpiga picha wetu*



*Wanafunzi washiriki wa mashindano ya Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) wamewasili Lindi wakiwa salama salmini.Picha na mpiga picha wetu.*

# TANZIA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu **Frank Fabian Chonya**, anasikitika kutangaza kifo cha Mwalimu **George Pauline Paul** wa Shule ya Msingi Nanganga kilichotokea tarehe 5, Machi saa 2: 30 usiku katika Hospitali ya St. Francis Ifakara alipokuwa anapatiwa matibabu.
Mazishi yatafanyika Ijumaa tarehe 8, Machi nyumbani kwao Dumila, Morogoro.

Bwana ametoa, Bwana ametwaa
Jina lake lihimidiwe.



ruangwadc www.ruangwadc.go.tz

# TANZIA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu **Frank Fabian Chonya**, anasikitika kutangaza kifo cha Mtumishi wake **Neema Peter Buhimu** aliyekuwa Mtendaji wa Kijiji cha Mihewe kilichotokea tarehe 30, Mei 2024 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alipokuwa anapatiwa matibabu.
Taarifa zaidi kuhusu mazishi, tutaendelea kujulishwa.

Bwana ametoa, Bwana ametwaa



# Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Afanya Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo



*Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa (Kushoto) Ndugu Frank Chonya akiambatana na Wataalamu wa Halmashauri wamefanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya maendeleo ya Halmashauri leo Juni 27, 2024. Picha na mpiga picha wetu.*

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Chonya akiambatana na Wataalamu wa Halmashauri wamefanya ziara ya ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa ndani ya Halmashauri, ziara hiyo imefanyika leo Juni 27, 2024.

Mkurugenzi na timu yake wametembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba ya walimu unaoendelea shule ya msingi Mmawa iliyopo kijiji cha Mmawa Kata ya Nandagala ambapo ujenzi wa boma umekamilika, amekagua mradi wa umaliziaji wa bwalo la shule ya sekondari Mary Majaliwa wenye thamani ya shiling 44,000,000/= ,amekagua mradi wa ujenzi wa mashimo 10 ya choo unaendelea shule ya msingi Mbuyuni wenye thamani ya shilingi 34,171,506.20/=

,Umaliziaji wa kituo cha Afya Mbuyuni kilichopo kitongoji cha Mbuyuni chenye thamani ya shilingi 67,000,000/= ambapo uwekaji wa madirisha, milango, umeme na mifumo ya maji unaendelea, umaliziaji wa Zahanati ya kijiji cha Namkatila wenye thamani ya shilingi 12,224,350/= , ujenzi wa kisima cha Zahanati ya Kijiji cha Mihewe chenye thamani ya shilingi 9,065,450/= ambapo ujenzi unaendelea.

Kamati pia imetembelea mradi wa umaliziaji wa kituo cha Afya Nangurugai wenye thamani ya shilingi 91,000,000/= na mradi wa umaliziaji wa kituo cha afya Narungombe wenye thamani ya shilingi 81,000,000/=

## Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Afunga Kikao cha MPDSR Wilaya ya Ruangwa

Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Bi. Zuwena Omary amefunga Kikao cha Mkoa cha uchambuzi wa vifo vya wakina mama wajawazito na watoto ( MPDSR) katika Wilaya ya Ruangwa.

Kikao kilianza kufanyika Juni 24, 2024 na kumalizika leo Juni 26, 2024 ambapo kimkoa kimefanyika katika Wilaya ya Ruangwa na kimefanyika katika ukumbi wa shule ya awali na msingi Wonder Kids.

Aidha, Bi. Zuwena amewataka Madaktari wa Mkoa wa Lindi kuunda kundi la madaktari bingwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ili kutoa huduma ya afya kwa jamii katika maeneo mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Bi. Zuwena amewaomba Wataalam wa afya kufanya kazi kwa moyo mkunjufu ili kuokoa uhai wa wagonjwa mbalimbali hususani wakinamama wajawazito na watoto.

Nae, Mganga mkuu wa Mkoa wa Lindi Dkt. Kheri Kagya ameushukuru uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa mapokezi na maandalizi mazuri ya Kikao hicho cha MPDSR.



# Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ruangwa Atamatisha Mafunzo ya Kuwajengea Wanawake Uwezo Kiuchumi



*Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ruangwa Ndugu Rashidi Namkulala akitoa mafunzo ya kuwajengea wanawake uwezo kiuchumi na uongozi katika kata ya Nachingwea WIlaya Ruangwa. Mafunzo hayo yametamatika leo Juni 30, 2024. picha na mpiga picha wetu*

Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ruangwa Ndugu Rashidi Namkulala ametamatisha mafunzo ya kuwajengea wanawake uwezo kiuchumi na uongozi leo Juni 30, 2024 katika Kata ya Nachingwea wilayani Ruangwa.

Mafunzo haya ni Mradi uliofadhiliwa na Shirika la @unwomen wenye lengo la kuongeza uelewa na ushawishi kwa viongozi wa dini, viongozi wa mila na wananchi kwa ujumla katika kumkomboa mwanamke kiuchumi na kumuwezesha kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Aidha, Ndugu Namkulala ameongeza kwa kusema kuwa uwazi, uaminifu, imani na uvumilivu ni chachu ya maendeleo katika familia.



# Watumishi wa Afya Ruangwa Waagizwa Kuhakikisha Dawa Haziishi Muda Wake Kabla ya Matumizi

Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Bi. Zuwena Omary amewataka watumishi wa afya kuhakikisha dawa haziishi muda wake kabla ya matumizi.

"Katika matumizi ya dawa zingatieni sana muda wake wa mwisho wa matumizi, kama kuna zile dawa ambazo zinakaribia muda wake kuisha ni lazima zianze kutumika hizo ili ziishe au ni vyema kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili kama kuna uwezekano zisambazwe katika maeneo tofauti tofauti na si kukaa nazo tu mpaka muda wake wa matumizi unaishia wakati huo nyie wataalam wa Kituo au Hospitali husika mnazitazama, kuna wagonjwa wengi sana wanazihitaji hizo dawa ili waweze kupona" Amesema Bi. Zuwena

Ameyasema hayo leo Juni 26, 2024 katika Kikao cha Mrejesho wa Usimamizi Shirikishi Sekta ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya Ruangwa kilichofanyika katika ukumbi wa shule ya awali na msingi Wonder Kids.

Katika hotuba yake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi Dkt. Kheri Kyaga ameupongeza uongozi na watumishi sekta ya Afya, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuwataka kuboresha mapungufu yaliyopo katika sekta hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Ndugu Frank Fabian Chonya amemhakikishia Mganga Mkuu wa Mkoa kuyafanyia kazi mapungufu hayo ili kuimarisha sekta ya afya walayani Ruangwa.



*Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Bi. Zuwena Omary amewatakaakizungumza na wa afya wa Wilaya ya Ruangwa kuhakikisha dawa haziishi muda wake kabla ya matumizi. leo Juni 26, 2024 katika Kikao cha Mrejesho wa Usimamizi Shirikishi Sekta ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya Ruangwa kilichofanyika katika ukumbi wa shule ya awali na msingi Wonder Kids.Picha na mpiga picha wetu*

# Mkuu wa Wilaya Ya Ruangwa Aridhishwa na Watumishi Sekta ya Afya Mkoa wa Lindi



*Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma akizungumza na watumishi wa afya katika kikao cha Mkoa cha uchambuzi wa vifo vinavyotokana na uzazi kwa mama na mtoto kilichofanyika Juni 24, 2024 wilayani Ruangwa na kubainisha kuwa vifo vimepungua sana ukilinganisha na mwaka 2015/2016. Aidha amewapongeza watumishi wa afya sana. Picha na mpiga picha wetu.*

Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma ameridhishwa na ufanyaji kazi wa watumishi sekta ya afya Mkoa wa Lindi katika kuzuia na kupambana na vifo vya watoto wachanga na mama wajawazito.

Ameyabainisha hayo katika kikao cha Mkoa cha uchambuzi wa vifo vinavyotokana na uzazi kwa mama na mtoto kilichofanyika Juni 24, 2024 wilayani Ruangwa na kubainisha kuwa vifo vimepungua sana ukilinganisha na mwaka 2015/2016.

"Vifo vilikua 556, kama nchi tumefanikiwa kushusha hadi kufikia 104 huku watoto wachanga katika vifo 100 walifariki 67 tu kitaifa, ila kimkoa tumetoka vifo 47 vya wazazi mwaka 2021 hadi kufikia vifo 32 mwaka 2022 huku Kwa upande wa watoto wachanga vifo viliongezeka kutoka vifo 172 hadi 243 mwaka 2023 " Amesema Ngoma.

Kwa upande wake, Mganga mkuu wa Mkoa wa Lindi Dkt. Kheri Kagya amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

kwa uwekezaji mkubwa sana katika sekta ya afya nakupelekea kupunguza vifo vya mama na mtoto, huku akibainisha kuwa zaidi ya 97% ya wakina mama Mkoa wa Lindi wanajifungulia hospitali na siyo majumbani kama ilivyokuwa zamani.

## Benki ya NMB Yafanya Kikao na CMT Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa

Benki ya NMB tawi la Ruangwa imefanya kikao na timu ya Menejimenti ya Wilaya ya Ruangwa (CMT), leo Juni 28, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

Lengo kuu la kikao hicho ni kudumisha uhusiano mzuri kati ya Benki ya NMB na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, ambapo NMB imemtambulisha meneja wake mpya wa tawi la Ruangwa kwa Menejimenti ya Halmashauri sambamba na hayo pia NMB ilikuwa na lengo la kutoa elimu kwa watumishi kuhusu umuhimu wa kuweka akiba na upatikanaji wa mikopo.

Aidha, Katika kikao hicho viongozi wa NMB wametoa elimu kuhusu faida za kuweka akiba kwa watumishi wa umma na jinsi wanavyoweza kunufaika na mikopo inayotolewa na benki hiyo. Kikao hicho kimejadili pia njia mbalimbali ambazo benki inaweza kushirikiana na Halmashauri katika miradi ya maendeleo na kuboresha huduma za kifedha kwa wananchi.

Sambamba na hayo, wamejadili mbinu za kuboresha ushirikiano katika kutoa huduma bora kwa wateja na kuhakikisha kuwa watumishi wanapata elimu stahiki kuhusu masuala ya kifedha, ikiwa ni pamoja na matumizi bora ya mikopo na mbinu za kuwekeza ili kujenga maisha bora ya baadae.

Ikumbukwe Benki ya NMB imekuwa na kawaida ya kufanya vikao na halmashauri vyenye lengo la kujenga mahusiano kati ya NMB na Halmashauri,

na kuweka msingi mzuri wa ushirikiano endelevu ambao utawasaidia watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na wananchi wake kwa ujumla.......



*Benki ya NMB tawi la Ruangwa imefanya kikao na timu ya Menejimenti ya Wilaya ya Ruangwa (CMT), leo Juni 28, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. wamejadili mbinu za kuboresha ushirikiano katika kutoa huduma bora kwa wateja. picha na mpiga picha wetu.*

# Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Azindua Huduma ya Umeme Kijiji cha Mmawa

Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma ametembelea kijiji cha Mmawa kilichopo kata ya Nandagala Wilaya ya Ruangwa leo Juni 27, 2023 na kuzindua huduma ya umeme.

Ziara hio ya mkuu wa Wilaya imehusisha Mwenyekiti wa Halmashari, Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri na Wataalamu wa Halmashauri.

Aidha Mhe. Ngoma amewasisitiza wananchi wa Mmawa kuchangamkia fulsa hii ya umeme ili waweze kufanya uwekezaji kijijini kwao.

“Mimi niwahakikishieni Fulsa zilivyo uwezi kuziona wakati zinakuja utakuja kuziona wakati zimekwisha tokea mimi nitarudi hapa miezi sita ijayo watu hamtaamini macho yenu hapa kutakuwa na maduka mengi, saluni, mashine za kuchomelea vyuma kwahiyo changamkieni fulsa wekezeni kwa fulsa hii ya umeme mliyoipata hususani ninyi vijana changamkeni”.

Aidha Mhe. Ngoma amewasisitiza wanakijiji cha Mmawa kushiriki kwenye MMawa Marathon itakayofanyika



**Vifo vilikua 556, kama nchi tumefanikiwa kushusha hadi kufikia 104 huku watoto wachanga katika vifo 100 walifariki 67 tu kitaifa, ila kimkoa tumetoka vifo 47 vya wazazi mwaka 2021 hadi kufikia vifo 32 mwaka 2022 huku Kwa upande wa watoto wachanga vifo viliongezeka kutoka vifo 172 hadi 243 mwaka 2023**

**— Ngoma —**

## Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Aipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa Kupata Hati Safi

Katibu Tawala Mkoa wa Lindi Bi. Zuwena Omari ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa kupata hati safi miaka mitano mfululizo kutoka mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2022/2023.

Pongezi hizo zimetolewa leo Juni 26, 2024 katika Mkutano maalum wa Baraza la Madiwani la kupitia na kujadili hoja za Mkaguzi wa hesabu za mwisho za mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha. Bi Zuwena amewasisitiza Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kuilinda hati safi hiyo ili isije kuwa hati yenye mashaka au hati mbaya kwa mwaka wa 2023/2024.

Awali akiwasilisha taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali za Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa zinazoishia tarehe Juni 30, 2022/2023 Ndugu Donald Malick kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi wa hesabu za Serikali Mkoa wa Lindi, amesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ilikuwa na hoja za ukaguzi 25 kati ya hizo 13 zimeshatekelezwa na kufungwa, hoja 10 zipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji na hoja 2 hazijatekelezwa. Kwa Upande wa Mfuko wa pamoja wa Afya (Basket Fund) kulikuwa na hoja 3 kati ya hizo 2 zimefungwa na hoja 1 ipo katika hatua ya utekelezaji, halikadhalika Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu kulikuwa na hoja 3 ambapo 1 imetekelezwa na 2 zipo katika hatua za utekekezaji. Kutokana na hali hiyo Bi. Zuwena amewataka Madiwani na Watendaji wa Halmashauri kuharakisha kutafuta vielelezo vya hoja zilizobakia na kuziwasilisha ofisi ya Mkaguzi ili hoja hizo zifungwe.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa Mhe. Hassan Ngoma ameahidi kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha mwaka ujao wa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa isiwe na hoja za ukaguzi.

Nae, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mhe. Andrew Chikongwe ametoa pongezi kwa Madiwani kwa kusimamia fedha za Halmashauri hasa upande wa miradi ya maendeleo na kutoa wito kuendelea kushirikiana ili kuendelea kufanya mambo mazuri na ya kuleta maendeleo katika Kata na Halmashauri kwa ujumla.



***Waheshimiwa Madiwani wa Ruangwa wakiwa kwenye Kikao maalum wa Baraza la Madiwani la kupitia na kujadili hoja za Mkaguzi wa hesabu za mwisho za mwaka wa fedha 2022/2023 leo Juni 26, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa. Picha na mpiga picha wetu.***

## Wanawake Kata ya Mandawa Wapewa Mafunzo Kujikomboa Kiuchumi




Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ruangwa Ndugu Rashidi Namkulala aongoza mafunzo ya kumkomboa mwanamke katika sekta ya kiuchumi na kushiriki katika nafasi za uongozi na kusema kuwa kwenye ukombozi wa mwanamke katika sekta yoyote mwanaume hawezi kusahaulika.

Ameyasema hayo leo Juni 29, 2024 katika Kikao cha Mafunzo cha kuwajengea wanawake uwezo kiuchumi na uongozi kilichofanyika shule ya msingi Mandawa wilayani Ruangwa.

Aidha, Kikao hicho kilihusisha majadiliano ya namna gani mwanamke atakombolewa katika sekta ya uchumi na kuwania nafasi mbalimbali za uongozi. Kwa upande wao wanaume ambao walishiriki kikao hicho walitoa maoni yao kuhusu changamoto wanayoipata baada ya kuwawezesha wanawake ni kwamba wanawake wakiwezeshwa wanaanza kuwa jeuri na wanakuwa hawatawaliki tena.

Nao, wanawake kwa upande wao walitoa maoni yao ya kwamba wanaume hawawaruhusu wanawake hao kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo na kuwania nafasi za uongozi kwa sababu ya wivu wa kimapenzi

Katika hatua nyingine, wanaume na wanawake hao wamefikia muafaka wa kukubaliana ya kwamba katika familia ili maendeleo yapatikane pande zote kikubwa ni uwazi, uaminifu, imani na uvumilivu.

**Wilaya ya Ruangwa imeanzishwa mnamo mwaka 1995 wakati wa Raisi wa awamu ya pili Hayati Ally Hassani Mwinyi, nakuzinduliwa rasmi mwaka 1999 wakati wa Raisi wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa.**
**Wilaya ya Ruangwa inapatikana ndani ya Mkoa wa Lindi katika majira nukta -10.0809° S, 38.9401° E ipo umbali wa kilometa 150 kutoka makao makuu ya Mkoa , ina Vijiji 90, Kata 22, Vitongoji 150 na idadi ya watu wapatao 185,573, kati ya hao 91,469 ni Wanaume na 94,104 ni Wanawake kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 .**

# TIMU YA WAHARIRI

## WAHARIRI

MPETA KOBA
NYAMBITA MAGOMA

## MPIGA PICHA

MPETA KOBA

## MWANDISHI

ADELINA KASPALI

## MSANIFU KURASA

NYAMBITA MAGOMA

# JARIDA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

**Ruangwa kwa Mendeleo Inawezekana Timiza Wajibu wako**

ruangwadc

www.ruangwadc.go.tz

ruangwadc

Limeandaliwa na kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa
Barua pepe: ded@ruangwadc.go.tz
Tovuti: www.ruangwadc.go.tz
S.L.P 51, Ruangwa
Fax: +25532933212

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA